



**MINISTÈRE
DE L'EUROPE
ET DES AFFAIRES
ÉTRANGÈRES**

*Liberté
Égalité
Fraternité*

DIRECTION GÉNÉRALE DE L'ADMINISTRATION
ET DE LA MODERNISATION

DIRECTION DES RESSOURCES HUMAINES

Sous-direction de la Formation et des Concours

Bureau des Concours et Examens professionnels
RH4B

**CONCOURS EXTERNE ET INTERNE POUR L'ACCÈS A L'EMPLOI DE
CONSEILLERE/CONSEILLER DES AFFAIRES ÉTRANGÈRES
(CADRE D'ORIENT)
AU TITRE DE L'ANNÉE 2022**

ÉPREUVES ÉCRITES D'ADMISSIBILITÉ

Mercredi 8 septembre 2021

SWAHILI

Durée totale de l'épreuve : 3 heures

Coefficient : 2

Toute note inférieure à 10 sur 20 est éliminatoire

Barème de notation : composition en swahili 12 points ; traduction en français 8 points



TRADUCTION EN FRANÇAIS

Traduction en français d'un texte rédigé en swahili

TEXTE AU VERSO

Uchaguzi mkuu Ethiopia: je ni fursa ya kuzaliwa upya kwa demokrasia au kuendelea kwa mizozo?

Ethiopia inajiandaa kufanya kile ambacho waziri mkuu wake anakieleza kama jaribio la kwanza la nchi hiyo kufanya uchaguzi mkuu huru na wa haki, lakini unafanyika wakati nchi hiyo ikiwa katika usalama wenye mashaka, vyama vya upinzani vikisusia uchaguzi huo na jimbo lake la Tigray ambalo sio tu kitovu cha mapigano, bali liko kwenye hatari kubwa ya baa la njaa.

Uchaguzi huu unatoa picha ya hatma ya Ethiopia - nchi ambayo sio tu inahaha kujitambulisha kama taifa linalokua kiuchumi barani Afrika, lakini pia taifa linalokua kwa kasi kidemokrasia, kutaka kuhitimisha miongo kadhaa ya uchaguzi uliojaa udanganyifu. (...)

Waziri mkuu kijana wa Ethiopia, Abiy Ahmed alipata tuzo ya amani ya Nobel mwaka 2019, kama sehemu ya kutambua mchango wake (...) kusaidia kupunguza ama kuondoa migogoro ya kikabilia nchini humo. Miaka miwili baadae, unaweza kuanza kuhoji kama kweli lengo la Abiy la kufanya mabadiliko nchini Ethiopia liko kwenye mwelekeo sahihi.

Hakuna shaka hata kidogo kwamba Bwana Abiy na chama chake kipya cha Prosperity kilichozaliwa kutoka chama tawala cha EPRDF, atashinda uchaguzi mkuu huo, na kumuwezesha kuwa na majukumu makubwa ya kusimamia na kutekeleza sera yake ya umoja inayofahamika kama 'tuje pamoja" (medemer) (...)

Tahadhari ya baa la njaa

Serikali ya Ethiopia inashikilia msimamo wake kwamba, kutofanyika uchaguzi katika eneo lililokumbwa na machafuko la Tigray ni jambo la bahati mbaya, licha ya kwamba eneo hilo lina viti vichache bungeni. Jimbo hilo la Tigray litafanya uchaguzi wake pale machafuko yatakapokoma na hali ya mambo kurejea kawaida.

Jumuiya ya kimataifa imeonya kwamba, eneo hilo limekumbwa na baa la njaa, lakini serikali inasisitiza kwamba, si kweli, eneo hilo halina njaa. Lakini pia kuna wasiwasi wa hali ya usalama katika maeneo mengi ya Ethiopia - kwa mfano Afar, Somali, Amhara, Oromia, Harari, Benishangul-Gumuz, South Wollo na maeneo mengine. Karibu watu milioni mbili wamekimbia makazi yao huko Tigray na kukimbilia katika maeneo mengine kutokana na vita. Hali tete ya usalama huenda ikaathiri idadi ya wapiga kura watakojitokeza kupiga kura lakini pia ushiriki wa vyama mbalimbali vya siasa hasa vya upinzani katika uchaguzi huo. Lakini serikali inaweza kujipiga kifua ikisema uchaguzi huu unapaswa kutazamwa kwa jicho jema, kwa sababu unaonyesha kuna demokrasia kwa sababu unashirikisha vyama vya siasa zaidi ya 50. (...)

Mataifa ya Ulaya yanalaumiwa kwa kufumbia macho yanayoendelea Ethiopia

(...) Mataifa ya magharibi ambayo awali yalifurahia hali ya mambo Ethiopia na kiongozi huyo mshindi wa tuzo ya Nobel, yameanza kuonyesha kusikitishwa. (...)

Ni ngumu kufikiria kwamba kiongozi huyo wa Ethiopia amejiandaa kukwepa kile kilichotokea mwaka 1984, baa la njaa. Lakini wakosoaji wa Bwana Abiy wana wasiwasi na maamuzi yake ya mashaka ya namna alivyoshughulikia mzozo wa kidiplomasi dhidi ya mataifa ya Misri na Sudan kuhusu mto Nile, mapigano kwenye jimbo la Tigray na mzozo na majirani zake, Eritrea. (...) Waweza kusema kwa sasa barani Afrika hakuna nchi iliyo katika wakati mgumu kuhusu uchaguzi wake kama Ethiopia.